# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani, Buyu,
70490 Mjini Magharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/2025

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Ningependa kuanza kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu (S.W) Mwingi wa Rehema na Mwenye Kurehemu kwa kutujaalia uhai na uzima, na kutufikisha siku hii ya leo ili tuweze kutekeleza majukumu yetu ya Kikatiba ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi wewe kwa kunipa fursa hii ya kipekee ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa niaba ya Kamati ya Bajeti ili kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Mwelekeo wa Hali Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inatokana na matakwa ya Kanuni ya 93(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la Mwaka 2020). Kanuni hii inaelekeza kuwa Mapendekezo ya Mwelekeo wa Mpango wa Taifa yawasilishwe katika Kamati ya Bajeti kabla ya kuwasilishwa katika Baraza kwa ajili ya majadiliano na kupitishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kukuarifu kwamba Kamati ya Bajeti imetimiza wajibu wake kikamilifu kwa kuzingatia kanuni husika. Tumepokea waraka wa Mwelekeo wa Mpango wa Taifa na tumefanya majadiliano ya kina na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango. Tumezingatia pia Kanuni ya 93(4) kwa kuwaalika Wenyeviti wa Kamati za Kudumu na wadau mbalimbali kushiriki katika mchakato huu. Wadau hawa walitoa maoni yao muhimu kuhusu taarifa hii, ambayo yamechangia sana katika kuimarisha mwelekeo wa mpango wa taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Shukrani zangu za dhati ziende kwa Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano wao. Walifika mbele ya Kamati ya Bajeti na kutoa maoni yao ya muhimu, ambayo yamechangia sana katika kuimarisha mwelekeo wa mpango wa taifa. Pia ningependa kuwashukuru wadau wote waliyokuja katika kikao cha Kamati yetu. Tunathamini sana muda wao na michango yao muhimu. Maoni yao yamezingatiwa kwa makini wakati wa majadiliano na Serikali na wakati wa kuandaa hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** Mafanikio ya hotuba hii yanatokana kwa kiasi kikubwa yametokana na michango ya Wajumbe wa Kamati ya Bajeti. Ninawapongeza kwa dhati kwa mashirikiano yao, ambayo yaliwezesha utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa ufanisi mkubwa. Kwa ruhusa yako, naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:

1. Mhe. Mwanaasha Kh. Juma — Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Soud Nahoda Hassan — Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Abdala Mussa — Mjumbe
4. Mhe. Mohamed Mgaza Jecha — Mjumbe
5. Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad — Mjumbe
6. Mhe. Rukia Omar Ramadhan — Mjumbe
7. Mhe. Suleiman Masoud Makame — Mjumbe
8. Mhe. Yussuf Hassan Iddi — Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Sekreteriati ya Kamati ya Bajeti. Ushirikiano wao mzuri Pamoja na ushauri wao umekuwa muhimu sana katika kuhakikisha mafanikio ya Kamati. Kwa ruhusa yako, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:

1. Ndg. Asha Said Mohamed — Katibu
2. Ndg. Abass Vuai Mohammed — Katibu
3. Ndg. Husna Rajab Othman — Katibu
4. Ndg. Shaib Fadhil Shaib — Katibu

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi huo, ningependa sasa kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kamati kuhusu Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025.

## TATHMINI YA MWENENDO WA HALI YA UCHUMI KWA NUSU MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonesha hadi kufikia Disemba, 2023, Uchumi wa Zanzibar umefikia wastani wa asilimia 7.6 kutoka wastani wa asilimia 6.3 mwaka 2022. Mwenendo wa ukuaji wa Uchumi wa Zanzibar unapimwa kwa kuangalia viashiria vya hali ya uchumi. Baadhi ya viashiria hivyo ni pamoja na ukuaji wa uchumi, mfumko wa bei, Mwenendo wa Sarafu. Ukuaji huu umechangiwa na uingiaji wa watalii na uwekezaji, kuimarika kwa shughuli za uvuvi, sekta ya huduma pamoja na kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa lengo la kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuweka mikakati ya kufikia Maendeleo ya Uchumi jumuishi na endelevu kwa kuimarisha sekta ya uvuvi, kilimo, biashara kwa kuanzisha sera ambazo zitakwenda kuimarisha sekta hizo kwa kuongeza kuinua hali za wananchi kiuchumi, kuongeza uwekezaji, kukuza ajira na hatimae kuongeza mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Mfumko wa Bei za bidhaa na huduma umefikia wastani wa asilimia 6.5 kipindi cha Julai – Disemba 2023 kutoka wastani wa asilimia 6.6 kwa mwaka 2022 kwa kipindi kama hicho. Kupungua kwa mfumuko wa bei kumetokana na kupungua kwa bei kwa baadhi ya bidhaa zisizo za chakula.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kudhibiti mfumko wa bei kuendelea kushuka kwa haraka Serikali inapaswa kuimarisha sekta mbalimbali zitakazozalisha bidhaa kwa wingi nchini ili kupunguza utegemezi wa uagizaji hususan kwa zile bidhaa ambazo tunaweza kuzizalisha nchini mwetu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea na hatua za udhibiti wa bei kwa kupitia Taasisi zake zinazohusika na utekelezaji huo kwa kuongeza juhudi za kuhakikisha mfumko wa bei unadhibitiwa na kuwa wenye kutabirika pamoja na kuweza kusaidia ukuaji wa uchumi kwa kuongeza kasi ya uzalishaji wa bidhaa na huduma.

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusu thamani ya nakisi ya biashara imeongezeka na kufikia TZS 818.4 bilioni ikilinganishwa na TZS 672.7 bilioni katika kipindi cha Julai -Disemba 2023. Kuongezeka kwa nakisi ya biashara kumesababishwa na kuongezeka kwa uingizaji wa nishati ya mafuta kufikia TZS 368.3 bilioni kutoka TZS 304.2 bilioni kwa kipindi kama hicho mwaka 2022.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, sehemu kubwa ya usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi unabebwa na zao la karafuu hali ambayo inapelekea kuwa na nakisi kubwa ya urari wa biashara kwa kushuka kwa usafirishaji wa zao la karafuu kutoka tani 3850 hadi tani 1405. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali katika kudhibiti nakisi ya biashara ni vyema kuangali mazao mengine ambayo yataweza kuuzika nje ya nchi ili kudhibiti nakisi hiyo pamoja na kuendelea kuwavutia wawekezaji ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa ndani ya nchi na kuuza bidhaa hizo katika masoko ya nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa kasi ya Uingiaji wa Watalii, imeripotiwa kwamba idadi ya watalii walioingia nchini katika kipindi cha Julai-Disemba mwaka 2023 wamefikia watalii 356,459 kutoka watalii 345,300 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Ongezeko hili limesababishwa na jitihada kubwa zilizochukuliwa na Serikali kwa kuitangaza Zanzibar kimataifa, kuendelea kuimarisha hali ya amani na utulivu nchini, kuongezeka kwa wakala wa usafirishaji watalii pamoja na kuitangaza Zanzibar kiutalii kupitia maonyesho ya nje na ndani ya nchi kwa kufanya makongamano ya kibiashara na uwekezaji katika mataifa mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo lakini pia inaitka Serikali itimize kwa haraka azma yake ya kuhakikisha Sekta ya Utalii inaimarika katika kisiwa cha Pemba na kukuza uchumi wa kisiwa hicho. Jambo hili litaisaidia kuongezeka kwa mchango wa Sekta ya Utalii katika Pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mwenendo wa Sarafu ya Tanzania, Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani na sarafu nyingine Duniani imeendelea kuwa tulivu kwa kuendelea kuwepo kwa akiba ya fedha za kigeni, ambapo hadi kufikia Disemba 2023, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa ni Dola za Kimarekani Bilioni 5.5. Hivyo, ni muhimu kwa Serikali kujitahidi kupunguza manunuzi ya bidhaa na huduma kutoka nje ili kuepuka kushuka kwa thamani ya sarafu na badala yake kuongeza uzalishaji utakaozidisha kiasi cha bidhaa zitakazouzwa nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Miongoni mwa sababu nyengine ambazo zimepelekea hali ya Sarafu ya Tanzania kuwa tulivu ni Serikali kuendelea kuweka sera madhubuti za uzalishaji wa ndani ili kuongeza usafirishaji wa bidhaa kutoka ndani na kusafirishwa nje ya nchi ili kuimarisha sarafu ya Tanzania na kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni.

**Mheshimiwa Spika**, Kama tunavyojua uimara wa shilingi unategemea kiasi cha bidhaa na huduma zinazouzwa nje ya nchi pamoja na thamani ya mauzo hayo. Hivyo, Kamati inaendelea kuisisitiza Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kuendelea kuwa na mashirikiano ya karibu na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) katika kudhibiti sarafu ya Tanzania kwa kuendelea kushirikisha benki za biashara, maduka ya kubadilisha fedha za kigeni pamoja na wadau wengine katika kusimamia sheria, miongozo ya fedha kigeni nchini pamoja na kanuni.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA NUSU MWAKA WA FEDHA 2023/2024 (JULAI– DISEMBA 2023)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipopitia Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2023/2024 imebaini kuwa, katika mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya TZS 1,514.79 bilioni zilipangwa kutumika kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2023, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2023/2024 unaonesha kiasi halisi cha fedha ambacho kimetumika ni jumla ya TZS 843.47 bilioni sawa na asilimia 108.77 ya lengo la kutumia TZS 692.43 bilioni kwa kipindi hicho na sawa na asilimia 50 tu ya lengo la TZS 1,514.79 biloni kwa mwaka mzima.

**Mheshimiwa Spika**, Tathmini hii inaonesha ni kiasi kikubwa cha fedha ambacho kimetumika katika kutekeleza miradi na programu mbali mbali kuliko vile ilivyotarajiwa kwa kipindi cha tathmini. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii ya kuleta maendeleo kupitia miradi ambayo inaendelea kutekelezwa. Ni matumaini ya kamati kuwa miradi hiyo itakamilika kwa wakati ili kukamilisha malengo yalikosudiwa ya kuleta maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Mbali na jitihada hizo ambazo Serikali inaendelea kuzichukua za kuhakikisha upatikanaji wa fedha za maendeleo unakuwa mzuri, bado kuna miradi ambayo utekelezaji wake sio wa kuridhisha. Mathalan, Mradi wa ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi wa Hospital za Wilaya na Mkoa. Mradi huu haujaanza licha ya kuwa umepangiwa kuteklezwa kwa mwka wa fedha 2023-2024.

**Mheshimiwa Spika**. Kamati imebaini kuwa fedha ambazo zimetumika katika miradi ya maendeleo ni kutokana na Bajeti ya ziada katika baadhi ya miradi ambayo inaendelea na utekelezaji. Wakati Kamati inatekeleza Majukumu yake ya kuangalia utekelazaji wa majukumu katika Taasisi za Serikali, imeona kuwa kuna miradi imetumia fedha zaidi ya kile kilichopangwa.

Hali hii imetokana na sababu mbali mbali ikiwemo kutokufanyika kwa upembuzi yakinifu wa kutosha katika miradi. Mfano, katika Programu ya ujenzi na ukarabati wa Ofisi za Serikali. Programu hii imetumia Zaidi ya fedha zake za awali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuwa na wataalamu wa kutosha wakati wa kufanya upembuzi yakinifu kabla ya kuanza Mradi ili kuepuka matumizi ya ziada katika kufanikisha utekelezaji wa miradi hiyo.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA JULAI - DISEMBA, 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali ilikadiria kukusanya na kutumia TZS 2840.85 bilioni, kati ya fedha hizo TZS 2,822.85 bilioni kutoka Serikali kuu na TZS 18.00 bilioni kutoka kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika utekelezaji wa kipindi cha Julai - Disemba, 2023/ 2024 makusanyo yamefikia TZS 1,660.67 bilioni sawa na asilimia 58 ya bajeti ya kukusanya TZS 2,840.85 bilioni kwa mwaka na asilimia 120 ya makadirio ya kukusanya TZS 1,383.70 bilioni ya kwa kipindi cha Julai – Disemba 2023. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza makusanyo kwani ni dhahiri kuwa, inazisimamia vyema taasisi zake zinazokusanya mapato pamoja na kuwepo kwa uwajibikaji wa walipa kodi katika kutimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa hiari.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti ina matarajio makubwa kuwa, ukusanyaji huo utaendelea kuimarika kwa robo mbili zilizobakia na kupelekea kuongezeka kwa mapato ambayo yataweza kusaidia katika kukamilisha utekelezaji wa shughuli za Serikali ikiwemo ukamilishaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi katika kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024 yamefikia jumla ya TZS 1, 437.36 bilioni sawa na asilimia 51 ya makadirio ya bajeti ya mwaka ya TZS 2,840.45 bilioni. Matumizi hayo yanajumuisha ulipaji wa mishahara kwa wafanyakazi wa Serikali, mishahara kwa ajili ya taasisi za Ruzuku, matumizi mengineyo ya mafungu na taasisi za Ruzuku, matumizi ya huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali na matumizi ya miradi ya Maendeleo. Kamati inaishauri Serikali kuendelea na mikakati yake ya kuimarisha mapato ili hatimae Serikali ifikie hatua ya kutumia mapato yake ya ndani kwa kiwango kikubwa zaidi

katika utekelezaji wa Bajeti na kuendelea kupunguza utegemezi wa bajeti kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kusimamia mwenendo wa ulipaji wa deni la taifa, Serikali imeanzisha Mfuko wa Kuhudumia Madeni (Debt Service Fund) kwa ajili ya kuhudumia mikopo ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa hatua hii. Katika kipindi cha Julai - Disemba 2023, Serikali ilipanga kuweka TZS 72 bilioni kwa ajili ya kuweka akiba katika kipindi hicho. Utekelezaji halisi umeonesha kuwa, fedha zilizowekwa ni TZS 90 bilioni ambazo zimevuka lengo. Hali hii inaonesha utayari mkubwa wa Serikali katika kulipa madeni yake wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati inaishauri Serikali kusimamia vyema kuhakikisha kuwa endelevu na kufikia malengo ya kuanzishwa kwake.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imeanzisha Mfuko wa Ustahamilivu wa Bei (Price Stabilization Fund) ili kuweza kusaidia kufidia gharama za ongezeko la bei. Kamati inaunga mkono uanzishwaji wa mfuko huu na inaishauri Serikali kwa upande mwengine, kufanya utafiti kuhusiana na uchambuzi wa bei " Price Structure Analysis " kwa bidhaa mbali mbali ili kuweza kutambua mambo yanayopelekea kupanda kwa gharama za bidhaa ikiwemo bidhaa za vyakula ambazo zina athari za moja kwa moja katika mfumko wa bei.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa mapato ya Mfuko wa Ustahamilivu wa Bei yanategemea kuchangiwa na mashirika mbali mbali na kwa kuwa mapato yaliyopatikana ya TZS 3.2 bilioni yamechangiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA) pekee. Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuendelea kuandaa utaratibu mzuri zaidi wa kuzishajihisha taasisi zinazojitegemea na mashirika kuuchangia mfuko huu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Julai - Disemba 2023/2024 kumekuwepo na mafanikio mbali mbali ikiwemo utekelezaji wa miradi ya kimkakati ikiwemo miundombinu ya barabara ambayo inarahisisha usafirishaji wa bidhaa na watu, kupatikana kwa miundombinu mizuri katika utoaji wa huduma za jamii hasa katika sekta ya elimu na afya, kupatikana kwa huduma za maji safi na salama pamoja na kupatikana kwa huduma za kiuchumi na kijamii kwa programu na miradi iliyokamilika.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine, katika utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha Julai - Disemba, 2023/2024 kumebainika changamoto mbali mbali katika utekelezaji ikiwemo

kupanda kwa bei ya bidhaa mbali mbali zikiwemo bidhaa za chakula ambazo zinaathiri sana wananchi hasa wa kipato cha chini, mahitaji makubwa ya bajeti ya mishahara ikilinganishwa na bajeti halisi inayoidhinishwa kunakotokana na kubadilika miundo ya taasisi, kuchelewa kuanza kwa baadhi ya miradi kutokana na kuchelewa kukamilika taratibu za awali pamoja na ongezeko la gharama kwa baadhi ya miradi na kusababisha kutokukamilika kwake.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kukabiliana na changamoto hizo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuchukua hatua mbali mbali za kukabiliana ni changamoto hizo ikiwemo kuandaa mipango na mikakati ya kuzitatua ili ziweze kutatuliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa hatua ambazo, Kamati inaishauri Serikali kuzichukua ni pamoja na kuendelea kuzisimamia kwa karibu taasisi zake hasa katika masuala ya ukusanyaji wa mapato na namna ya matumiz yanavyofanyika katika taasisi zake mbali mbali ili Serikali iweze kuondosha matumizi yasiyoleta tija. Aidha, katika kuhakikisha miradi inatekekezwa kwa muda uliopangwa, Kamati inaishauri Serikali kupitia taasisi zake kuendelea kusimamia ipasavyo michakato ya manunuzi ili kuondosha uwezekano wa matumizi mabaya ya fedha kupitia ununuzi.

## TATHMINI YA MATARAJIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa mwenendo wa makusanyo, Serikali inatarajia kukusanya TZS 2838.53 bilioni katika kipindi cha Julai 2023 hadi Juni 2024 sawa na asilimia 99 ya makadirio. Mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia jumla ya TZS 1,437.32 bilioni sawa na asilimia 101 ya makadirio ya bajeti. Aidha, Matumizi ya Serikali Kuu hadi kufikia Juni 2024 yanatarajiwa kufikia TZS 2,838.5 billioni sawa na asilimia 99 ya bajeti ya mwaka ya TZS 2,840.85 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Serikali imeshapanga mikakati madhubuti ya kukusanya mapato, kama vile utoaji wa risiti za kieletroniki, matumizi ya mfumo wa ZIDRAS, kuunganisha wafanya biashara na mfumo wa VFMS, uimarishaji wa elimu kwa walipa kodi pamoja na kuwa na watendaji wenye uweledi zaidi. Kamati inaishauri Serikali ihakikishe inaisimamia vyema mikakati iliyojiwekea kwa kuharakisha kuwaunga wafanyabiashara wote kwenye mifumo pamoja kuiunganisha mifumo mifumo yote muhimu kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato pamoja kupata taarifa.

## MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2024

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2024, kasi ya Uchumi wa Dunia inakadiriwa kukuwa kwa wastani wa asilimia 3.1 wakati uchumi wa nchi za Afrika Mashariki unatarajiwa kukuwa kwa wastani wa asilimia 5.8 ikiwa ni ongezeko la asilimia 1.1 kutoka mwaka 2023. Aidha, Uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.2 kwa mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 6.1 mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaisisitiza Serikali kuhakikisha inakuwa na mfumo utakaoweza kuunganishwa na makampuni yanayoleta watalii nchini ambao humaliza taratibu zote za ulipaji fedha katika nchi zao kwa lengo la kujua wageni watakaoingia nchini pamoja na kuweza kukusanya mapato kupitia watalii wa aina hiyo. Aidha, Kamati inaisisita Serikali kwa mara nyengine katika kuharakisha uungwaji wa mahoteli yote nchini katika mfumo kwa kuwa utalii ndio sekta inayochangia sehemu kubwa ya pato la nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2024/2025 umezingatia hali ya amani na utulivu nchini, ushirirki wa sekta binafsi kwenye uwekezaji, uzalishaji wa ndani, kuimarika kwa usimamizi wa sera za kifedha, kuimarika kwa upatikanaji wa nishati, pamoja na kuimarika kwa miundombinu mbali mbali. Aidha, shabaha ya ukuaji wa uchumi ili kufikia malengo ya Serikali imezingatia ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.2 kwa mwaka 2024 kutoka asilimia 7.1 kwa mwaka 2023, mfumko wa bei kubaki tarakimu moja, mapato ya kodi kufikia asilimia 23 ya pato la Taifa, uwiano wa deni na pato la taifa kufikia asilimi 13 kwa mwaka 2024/2025 kutoka asilimia 15 mwaka 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inasimamia vyema sera ya mpango wa ardhi kwa kuhakikisha miundombinu inayojengwa inakamilika nainatunzwa ili iweze kutumika kwa muda mrefu, Aidha, Serikali ihakikishe inajenga nyumba za bei nafuu kwa wananchi wake ili kuondoa utamaduni wa kila mtu kujenga hadi kwenye maeneo muhimu ya kilimo na vyanzo vya maji, kwa kufanya ivyo kutasaidia wananchi kuwekeza pesa zao kwenye miradi mengine ya kimaendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kasi ya mfumko wa bei Zanzibar inatarajiwa kupungua na kufikia wastani wa asilimia 5.5 kwa mwaka 2024 kutokana na Serikali kuweka mikakati ya kusimamia bei elekezi za bidhaa, kutekeleza vyema kwa sera ya fedha kupitia Benki Kuu ya Tanzania,

kuimarisha programu za kilimo, pamoja na kushajihisha uwekezaji wa viwanda nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua inazozichukua za kupunguza mfumko wa bei, aidha Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inatekeleza mikakati iliyojiwekea pamoja kuangalia uwezekano wa kuitumia ZSTC kwa kuagiza bidhaa kutoka nje na kuja kuwauzia wananchi kwa bei rafiki.

## TATHMINI YA MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2024/2025 umepangwa kutekeleza Programu na Miradi ambayo itajikita zaidi katika kuimarisha hali za wananchi, kukuza ajira na kuongeza mapato ya Serikali ili kuhakikisha maendeleo yanapatikana kwa haraka. Mpango huo wa Maendeleo, unategewa kutumia jumla ya TZS 2,455.68 bilioni sawa na asilimia 60.1 ya bajeti yote ya Serikali kwa mwaka 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuja na bajeti hii ya maendeleo, kwa sasa tupo katika njia sahihi, ili kufikia maendeleo tunayoyahitaji ni lazima bajeti ya kazi za maendeleo iwe kubwa kuliko bajeti ya kazi za kawaida.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa lengo la utekelezaji mzuri wa mpango wa maendeleo, Kamati inaishauri Serikali kuipa kipaumbele miradi inayoendelea yaani ishayoanza kutekelezwa ili ikamilishwe kwanza kabla kuanzwa kutekelezwa miradi mipya kwani kutaepusha kuongezeka kwa gharama. Ni jambo muhimu siku zote bajeti kuwa endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika upangaji wa maeneo ya kimkakati kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati inaishauri Serikali kuliweka eneo kuziimarisha kwa kuziongezea uwezo laini za umeme za chini ya bahari (submarine cables) zinazosafirisha umeme kutoka Dar es Salaam kwenda Unguja na kutoka Tanga kwenda Pemba. Hii ni kwa sababu ya kuongezeka matumizi ya umeme Zanzibar. Kwa mfano, laini mpya inayopeleka umeme Unguja ina uwezo wa kusafirisha kiasi cha megawati 100 na kiwastani matumizi yake yamefikia megawati 92 na laini kongwe ina uwezo wa kusafirisha kiasi cha megawati 40 matumizi yake yamefikia megawati 25. Hii inaonesha bado kiasi kidogo cha matumizi ambayo yatapelekea kuzidiwa kwa uwezo wa laini za kusafirishia umeme.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa laini inayopeleka umeme Pemba ina uwezo wa kusafirisha kiasi cha megawati 20 na matumizi ya kawaida yamefikia megawati 9 hadi 10 na baadhi ya siku kama vile siku za skukuu matumizi hufikia megawati 14.2. Ukiangalia miradi ya maendeleo inayotekelezwa Pemba kama vile Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Zanzibar, Miradi ya Ujenzi wa Viwanda mbali mbali pamoja na ujenzi wa hoteli za kitalii, bila ya shaka maeneo haya yataongeza matumizi ya umeme kwa Pemba. Hivyo, ili kufikia azma ya Serikali ya kuifungua kiuchumi Pemba, ni lazima suala la upatikanaji wa umeme wa ziada na wa uhakika liwe kipaumbele namba moja cha Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo la uimarishaji wa laini za umeme za chini ya bahari (submarine cables), Kamati inaishauri Serikali kuanza kufanya utafiti na tathmini ya kupata vyanzo vipya vya kuzalisha umeme. Vipo vyanzo ambavyo Kamati inaona vinaweza kuzalisha umeme kwa mazingira ya Zanzibar kama vile umeme wa jua, umeme wa joto la ardhi (geothermo), umeme wa upepo na umeme wa mawimbi ya bahari. Kupitia tafiti, Serikali itaweza kubaini ni chanzo kipi kitaweza kuzalisha umeme mwingi na wa uhakika zaidi na kwa gharama nafuu.

## TATHMINI YA MWELEKEO WA SURA YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali inatarajia kukusanya jumla ya TZS 4,085.80 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 43.8 ikilinganishwa na makadirio ya mapato ya mwaka 2023/2024 ya TZS 2,840.85 bilioni. Mapato hayo yanatarajiwa kuwa katika mgawanyo wa TZS 1,700.79 bilioni zinatarajiwa kukusanywa kutoka katika vyanzo vya ndani, TZS 1,580.00 bilioni mikopo ya ndani na nje na TZS 805.01 bilioni misaada na mikopo kutoka Washirika wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, Serikali inatarajia kutumia jumla ya TZS 4,085.80 bilioni yakiwemo matumizi ya kawaida ya TZS 1,630.12 bilioni na matumizi ya maendeleo ya TZS 2,455.68 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, Kamati inaishauri Serikali iendelee kusimamia ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi kwa

kuimarisha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji ili kukuza biashara ndogo na za kati kwa ukuaji endelevu wa uchumi utakaowezesha kuongezeka kwa wigo wa kodi pamoja na kuimarisha mazingira ya ulipaji kodi kwa hiari ikiwemo kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ili kuzipa mianya ya ukwepaji wa kodi, na kutoa elimu kwa umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inaishauri Serikali, utekelezaji wa bajeti ya mwaka ujayo ijikite zaidi katika kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa sambamba na kuimarisha hali ya uchumi wa wananchi, kuendelea kudhibiti kasi ya mfumko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuendelea na usimamizi na udhibiti wa fedha za umma, Kamati inaishauri Serikali kuainisha mapato mapato yatokanayo na gawio kutoka BOT, gawio kutokana na matumizi ya huduma za simu, gawio kutokana na tozo katika miamala ya simu pamoja na mgawo wa mikopo na misaada kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT).

**Mheshimiwa Spika,** Hatua nyengine ambayo Kamati yangu inaishauri Serikali ili kufikia lengo ukusanyaji wa mapato katika bajeti ya mwaka 2024/2025 ni Serikali kufanya tafiti na tathmini zinazolenga kuibua fursa mpya za mapato hususan yasiyo ya kodi na kuendelea kuimarisha mifumo ya mashirika na taasisi za umma ili kuongeza ufanisi na kujiendesha kibiashara na kuweza kutoa magawio stahiki. Aidha, Kamati inaisisitiza Serikali kufanya mapitio ya vyanzo vya mapato na mfumo wa ukusanyaji katika Serikali za Mitaa ili kuongeza mapato. Kamati inaamini kwamba, bado Serikali za Mitaa hazijapewa uwezo wa kukusanya mapato inavyotakikana hali ambayo inapelekea kukosa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na pia kuwepo na mianya mingi ya uvujaji wa mapato.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi, kwa wasaidizi wako na kwa watendaji wote wa Baraza. Ninashukuru sana ushirikiano wa karibu na miongozo mbalimbali mliyotupatia Kamati yetu katika kipindi chote cha kazi zetu. Pia ningependa kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza kwa kunisikiliza kwa makini na kwa utulivu. Zaidi ya hayo, ninawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa ushirikiano wao waliyonipatia wakati wote tuliyokuwa tukitekeleza majukumu ya Kamati yetu. Ni matumaini yangu kuwa mashirikiano haya yataendelea hata katika siku zijazo kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa lengo la hotuba hii ni kutoa tathmini katika mwelekeo wa bajeti ijayo na kuipa Serikali fursa ya kupokea maoni na ushauri wenye lengo la kuimarisha bajeti hiyo, Kamati yangu inatumai kwamba maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Bajeti, pamoja na Wajumbe wa Baraza lako utazingatiwa na Serikali wakati wa kuandaa bajeti ya mwaka 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, ningependa kuhitimisha hotuba hii kwa kuwaomba Wajumbe wa Baraza lako waichangie kwa kina taarifa hii ili kutoa fursa kwa Serikali, kupitia Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango, kuzingatia maoni na ushauri utakaotolewa katika mchakato wa kuandaa bajeti bora zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha.

Ahsante,

……………………

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**